# MTAALA WA UMILISI

7

2024

## SEKONDARI MSINGI

**KISWAHILI**

## MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

# SEHEMU A: KUSOMA

**Jibu maswali yote kwenye nafasi zilizoachwa wazi.**

Mawasiliano ni neno ambalo asili yake ni wasili. Wasili lina maana ya kufika kwa mtu, kitu, au jambo fulani baada ya mwendo au safari. Kwa hivyo kuwasiliana kuna maana watu, kitu au mambo kufikiana kutoka mahali.

Katika siku za jadi mawasiliano yalikuwepo lakini ya shida. Hata hivyo, watu waliwasiliana kwa kutumia moshi, ngomezi au kupiga mbiu. Mbinu hizi za jadi zilitumiwa baina ya vijiji ili kujulisha wanakijiji jambo la dharura au kuwajulisha jambo linguine lolote. Mbiu ilitumika kwa jambo la dharura. Njia za kusafirisha mizigo zilikuwa haba. Baadhi ya watu walitumia wanyama, kama fahali au farasi kukokotea mizigo yuao.

Siku hizi mawasiliano yamepanuka sana. Mawasiliano ya kisasa yanahusisha simu, mtandao, televisheni na wavuti. Mawasiliano ya kisasa yamefanya ulimwengu wa kisasa kuwa kijiji kimoja kikubwa.

Kwa kuzingatia maudhui haya, vyombo au njia kama redio, simu, waraka, ndege, meli, motokaa na wavuti vimepewa jina la vyombo vya mawasiliano. Hivyo basi yafaa tutathmini ni vipi vyombo au njia hizi hufanya kazi ya kuwasiliana na huwasilisha nini. Vyombo hivi vinaweza kuelezwa chini ya vichwa vitatu; usafiri, mazungumzo na picha. Vyombo mathalan baiskeli, ndege, meli na magari hufanya kazi ya kuwasafirisha watu kutoka janibu moja hadi nyingine. Watu wanaposafiri huwa wanasafirisha mali yao. Bidhaa kama kahawa, vyuma na mizigo mingine husafirishwa kwa meli, ndege na magari kupitia majini, hewani au barabarani.

Bandari, viwanja vya ndege na barabara zimeimarishwa ili kukuza uchumi na kuleta maendeleo. Anayesafirisha biodhaa fulani na wakati huo anatakikana kukusanya nyingine, inamlazimisha asiambatane na bidhaa hizo lakini ahakikishe zimewasili alikozikusudia. Hivyo basi njia nyingine ya mawasiliano ilivumbuliwa.

Njia hii ambayo ni mazungumzo hutumia vifaa kama barua, simu, barua pepe na kipepesi. Mtumiaji ataandika ujumbe na kuutuma kupitia shirika la posta au mashirika mengine ama mtandao. Yamkini ilihitajika kuweza kujibizana na kuulizana kati ya watu hao wawili ndipo simu ilipovumbuliwa na kumwezesha mtu kuzungumza na mwingine akiwa mbali sana. Watu huzungumza na kufahamiana. Ilipohitaji mtu kukiona kitu anachozungumzia ndipo ilibidi kuunda vifaa vya kuonyesha picha kama vile televisheni.

Ilikuwa fahari kubwa sana kwa Wakenya kuwasiliana na nchi ya Ghana wakati wa michuano ya mpira ya kuwania kombe la taifa bingwa Afrika. Wakenya waliweza kuiona michezo hiyo moja kwa moja ingawa kijiografia Kenya na nchi hiyo zina majire tofauti.


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Mawasiliano tuliyotaja ni vyombo vya ufundi vilivyoundwa lakini kunayo maswasiliano ya ana kwa ana. Mwalimu na mwanafunzi darasani huwasiliana kutumia midomo, mikono, macho, kichwa na ishara nyinginezo. Wanapofanya hivyo huwa wanaelewana.

Ndege kama kuku akihisi adui hufanya ishara au mlio fulani wa kutahadharisha viranga wakek katika michezo. Mwamuzi huwasiliana na wachezaji labda kwa kutumia firimbi au kipenga, kengelel au ishara za mkono. Kengele pia hutumiwa shuleni ili kuonyesha kukamilika kwa kipindi au kuhitajika mahali pengine.

Kwa muhtasari, mawasiliano hutumia chochote ilimradi ujumbe utokao kwa mtu, kitu au mahali fulani ufike panapotarajiwa.

**MASWALI:**

(i) Taja anwani faafu ya kifungo hiki. (alama 1)

**Mawasiliano**

(ii) Vyombo vya mawasiliano vimeleta manufaa gani katika maisha ya watu? (alama2)

- **Kuwasafirisha watu na bidhaa kwa upesi**
- **Kuwasilisha ujumbe/taarifa/habari**
- **Kuona matukio yakiwepo mbali**
- **Kuimarisha uchumi na maendeleo**

(iii) Mawasiliano yameelezwa katika vipenge vitatu. Vitaje. (alama3)

- **Usafiri**
- **Mazungumzo**
- **Picha**

(iv) Andika visa we (alama 2)

**(a) Televisheni –Runinga**
**(b) Waraka – Barua**

(v) Nini maana ya: (alama 2)

**(a) Ana kwa Ana – Hali ya kuwa mnaonana**

**(b) Ulimwengu umekuwa kijiji kimoja kikubwa – Mawasiliano yamerahisishwa sana ulimwenguni**


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

# SEHEMU B: SARUFI

(a) Taja aina mbili kuu za sauti za Kiswahili. (alama 2)

**Irabu**
**Konsonanti**

(b) Taja vigezo vitatu vinavyotumika kuainisha konsonati. (alama 3)

**- Mahali zinapotamkiwa**
**- Jinsi au namna zinavyotamkwa**

**- Mghuna au kutoghuna kwa wauti au mtetemko wa nyuzi za sauti**

(c) Taja aina mbili za konsonanti zenye aina ya vipasuo. (alama 2)

**|p|**
**|k|**

(d) Andika majukumu tatu ya lugha. (alama 3)

**- Lugha hutumika kwa mawasiliano**
**- Ni chombo kinachotusaidia kujieleza na kutoa mawazo yetu**
**- Lugha hujenga uhusianao baina ya watu**
**- Lugha huimarisha uhusiano kati ya jamii na jamii taifa**
**- Lugha ni kitambulisho cha taifa**

(e) Andika maneno yenya miundo ya silabi ifuatayo. (alama 3)

**KI (Konsonanti irabu) – Kitabu, baba, mama**

**KKI (Konsonanti, konsonanti, irabu) – Penda unga, panga**

**II (irabu) – Ua, Oa.**

(f) Bainisha man eno haya yanapatikana katika ngeli ipi? (alama 3)

**Ngoma – I -**
**Ukuta – U-Zi**
**Macho- li - Zi**
**Ugonjwa – ya**
**Mmea – U - I**
**Maiti – A – wa**

(g) Andika vinyume vya sentensi zifuatazo:- (alama 2)

(i) Mama anaanika nguo

**Mama anaanua nguo**

(ii) Baba anaenda sokoni.


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

**Baba anatoka sokoni**

(h) Kanusha sentensi zifuatazo. (2 mks)

(i) Mkulima analima shamba.

**Mkulima halimi shamba**

(ii) Mwanafunzi anasoma kitabu.

**Mwanafunzi hasomi kitabu**

(i) Onyesha Nomino (N), kitenzi ®, kielezi (E) Kiunganishi (U), na kivumishi (v) katika sentensi

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

hizi

(i) Mtoto anacheza vizuri.
**N T E**

(ii) Utacheza au utasoma?
**T U T**

(iii) Wanafunzi wawili wanalala.
**N V T**

(j) Toa neno kwa kila moja ya sauti ambatano zifuatazo.
**Nyw – Kunywa**
**Nd – Ndoo, kondoo**
**Ngw – jangwa**

(k) Onyesha silabi inayowekewa shadda kwenye maneno yafuatayo. (alama 4)
**Kara'tasi –**
**Sha'iri –**
**Baraba'ra(njia kuu)**
**'Mto –**

**l.** Sauti ni nini? (alama 2)
Ni mlio unaotokana na mgusano wa ala za kutammkia kinywani

**m.** Kuna sauti aina ngapi? Zitaje. (alama 2)
Kuna sauti aina mbili
Irabu/vokali na konsonanti

**n.** Akifisha sentensi hii:
Ann Musa musa unaitwa musa Ann na nani na mama (alama 3)
Ann: Musa! Musa! Unaitwa
Musa: Na nani?
Ann: Na mama

**o.** Hizi ni nomino za aina gani? (alama 4)
a. 'Oduor – ya pekee

b. 'Miti – kawaida/jumla

c. 'Mchanga – wingi

d. 'Jeshi – makundi


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

**p.** Fafanua vivumishi vilivyopigwa mstari. (alama 3)

a. Mtoto mwerevu amefuzu

Nomino kivumishi

b. Mahali gani hapa –

Kiulizi

c. Baba yangu ni huyu -

Kimilikizhi

**q.** Tumia kihusishi kifaacho kutoka jedwali kujaza pengo (kumbe, ala, alhamdulilah) (alama 1)

Nilikufikiria kuwa Rafiki mwema **kumbe** wewe ni adui mkubwa.

**r.** Jaza viambishi vifaavyo:- (alama 4)

a. Huyu ndiye aliye kuchunguza ulipotupa mawe.

b. Huu ndio mkuki uliorushwa.

**s.** Pambanua sentensi hii kwa njia ya mstari.

Mwanafunzi mwerevu husoma vitabu vingi. (alama 2)

N + V + T + N + V

**t.** Andika ka tika hali ya udogo

Nyumb a yangu ndogo lakini inawapangaji wengi. a (alama 2)

Kijumb change kidogo lakini vipangaji ni vingi

**SEHEMU YA C: ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

(i) Eleza maana ya Isimu jamii. (alama 2)

**Ni matumizi ya lugha katika jamii.**

(ii) Taja na ufafa ugha.

nue mambo/dhana nne zinazozingatiwa katika matumizi ya l (alama 8)

**(Mwanafunzi atoe maelezo)**

**Wahusika**

**Tabaka**

**Jinsia**

**Elimu**

**Umri**

**Wakati**

**Mahali**

**Uhusiano wao**

**Tukio lenyewe**



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

# SEHEMU D: KUSOMA

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuatia.**

Michuano ya mechi ya kutafuta timu bingwa katika mchezo wa kabumbu barani Afrika mwaka wa 2004 ilifanyika nchini Tunisia, iliyo janibu ya Afrika kaskazini. Mji mkuu wa Tunisia, Tunis ulikuwa mahali pa kila aina za **shamrashamra** kwa wenyeji na wageni. Michezo hii huandaliwa baada ya miaka miwili na huchukua siku kadha **mtawalia** ingawa panaweza kuwa na siku za mapumziko. Mji ulinadhifishwa na nyuga ziliandaliwa kwa michuano hiyo. Michuano hii ilishirikisa timu kumi na sita.

Mataifa yote thelathini na sita hayakushiriki yote kwa sababu ya kushindwa au nyinginezo. Timu zinazoingia katika kinyang'anyiro hicho hupatikana baada ya mashindano ya mchujo. Hapo, nchi hucheza mechi za nyumbani na zile za ugenini. Timu hizi huwa katika makundi tofauti. Washindi kutoka kila kikundi hushiriki mkondo wa pili ambao huwa wa mch

Madhumuni y ujo wa mechi za nyumbani na ugenini. goni mwa mataifa washiriki, kub duni, mitindo ya mavazi, vyaku a mechi hizi aghalabu huwa mengi: kuleta umoja mion utoka nje hasa mataifa ya Ula urudisha, kuleta ufahamikiano katika Nyanja za utama la i walioshiriki, na kadhalika. Mara nyingine ni mawindo ya timu k ya kutafuta wachezaji stadi. Miongoni mwa wachezaj

wamo wengi wanaochezea timu za nchi za Ulaya ambako wanapewa fulusi nyingi. Jambo hili hupokonya bara la Afrika talanta zake! Ukweli ni kwamba vilabu vya nje huwalipa wachezaji vizuri na vina usimamizi bora kuliko ilivyo katika nchi nyingi barani Afrika.

Usimamizi mbaya hufanya hali ya michezo kuzorota katika nchi za Afrika. Kuepukana na jambo hili lazima mashinani kuwe na vilabu vinavyosaidiwa na kamai au shirika linalohusinana na mchezo huu. Pia ni bora kuazisha kambi za vijana chipukizi ili kupata wachezaji watokaoinua timu ya taifa.

Michezo hii ya barani Afrika huwa kigezo cha ujuzi na umahiri wa wachezaji katika kusakata kabumbu. Aghalabu wachezaji hutuzwa kutokana na juhudi zao katika ngazi hii ya **kilele**. Kwa mfano, mchezaji aliyefunga mabao mengi au aliyeonyesha umahiri wa kipekee katika michuano hiyo hutuzwa medali.

Michuano hii huileta nchi andalizi faida nyingi. Kwa mfano, kuboreka kwa njia za mawasiliano, kupata wageni wanaotalii miongoni mwa mengine. Baadhi ya wageni hasa makocha huja kufanya ujasusi juu ya miamba wa bara hili ambao watamenyana nao katika michuano ya kuwania kombe la dunia inayofanyika baada ya kila miaka minne.

Nidhamu ni jambo linalotiliwa maanani sana katika shughuli hiyo. Wakati mwingine kwa sababu kadha wa kadha za kinidhamu, mchezaji wa timu fulani huweza kurudishwa nyumbani. Miongoni mwa makosa haya ni kutumia dawa za kuongezea misuli nguvu, kupigana na ulevi.

Mwisho wa kinyang'anyiro hiki Tunisia iliibuka timu bingwa na ilitunukiwa kombe, medali na kitita cha pesa.

1. **Maswali:**


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

(i) Taja faida tatu ambazo nchi andalizi ya mechi hizi za kandanda hupata (alama 2)

- Nchi hupata kuboreka kwa njia za mawasiliano

- Kupata wageni watalii

(ii) Kwa nini mchezaji hufukuzwa katika kampi? (alama 2)

- Kwa kukosa nidhamu kwa mfano kutumia dawa za kusisimua misuli aku kupigana au ulevi.

(iii) Sababu zi pi hufanya wageni kuja kutazama michezo hii? (ala ma 2)

Wageni huja kujiburudisha kuona mechi

- Ni ma windo ya wachezaji na timu za nje
- Kufah amu utamaduni wa Nyanja tofauti

(iv) Timu inayoibuka bingwa hupewa nini? (alama 2)

Timu bingwa hutunukiwa kombe, medali na kitita cha pesa.

(v) Eleza maneno haya kama yalivyotumiwa katika taarifa. (alama 4)

(a) Fulusi nyingi – Pesa nyingi

(b) Kabumbu – Soka, kandanda

(c) Shamrashamra – Kushughulikia mambo ya burudani

(d) Kuwania – kupigania


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes